NIPASHE UK 10.

# Wakulima mwani wapatiwa vipande 700,000 vya kamba

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dk. Rashid Tamatamah, amekabidhi vipande vya kamba za manila 700,000 kwa wakulima wa mwani katika Kijiji cha Songosongo, wilayani Kilwa, mkoa wa Lindi.

Akizungumza na wananchi wa Songosongo juzi, Dk. Tamatamah alisema serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi) imetoa kamba hizo, ili kuwawezesha wakulima wa mwani kwani kamba ilikuwa ni moja ya changamoto waliyokuwa wakikabiliana nayo.

Kamba hizi za manila (ambazo kila moja ina urefu wa mita 10) katika kilimo cha mwani, hufungwa katika vigingi na hutumika kwa ajili ya kuoteshea mwani ambapo mwani hufungwa katika kamba hizo zinazosaidia pia mwani kutochukuliwa na maji ya bahari pale panapokuwapo na wimbi.

Dk. Tamatamah alisema duniani kote kwa sasa mwani unalimwa kibiashara, hivyo mwani ni moja ya zao linalopewa kipaumbele katika wizara.

Katika kilimo cha mwani wakulima wanakutana na changamoto mbalimbali zikiwamo za ukosefu wa mitaji na masoko.

"Wizara kupitia sekta ya uvuvi imeanza kutoa kamba ambazo ni moja ya pembejeo muhimu kwa wakulima wa mwani ikiwa ni sehemu ya kuwawezesha wakulima hao kwa kuwapunguzia sehemu ya gharama za uzalishaji ili baadaye waweze kusimama wenyewe," alisema Dk. Tamatamah.

Pia, alisema kama wakulima watalima vizuri katika kamba moja ya mita kumi katika bamvua nne (miezi miwili), wanaweza kupata kati ya kilo 8-10, na kamba hizo walizopewa zinaweza kutumika kwa mwaka mzima. Lengo la wizara ni kusambaza kamba hizi kwa wakulima wa mwani maeneo yote Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa Dk. Tamatamah, ipo changamoto ya soko la mwani hasa kwenye bei kwani kwa sasa asilimia 90 ya mwani inauzwa nje ikiwa ghafi na ni asilimia 10 tu ndio inayotumika hapa nchini.

"Hivyo wizara kwa sasa inawahamasisha wakulima kujiunga katika vikundi na kuwaunganisha na taasisi za kifedha ili waweze kukopesheka na waweze kuanzisha viwanda vidogo vya kuchakata mwani ili kuuongezea thamani. Hii itasaidia kupunguza kiasi cha asilimia ya mwani inayokwenda nje ya nchi ikiwa ghafi na kusaidia kuongeza ajira," alisema.

Aidha, Tamatamah alisema zao la mwani linazo faida kubwa ikiwa ni pamoja na kuongeza kipato katika jamii za maeneo ya pwani hasa kwa kinamama, inaondoa umaskini lakini pia linaingiza fedha za kigeni.

Naye mkulima wa mwani, Mbimbisa Omary, alimshukuru Katibu Mkuu kwa kuwaletea vitendea kazi kwa ajili ya kilimo cha mwani.

Mbimbisa alisema kilimo cha mwani kinawasaidia mambo mengi ikiwa ni pamoja na kuwasomesha watoto, kununua chakula pamoja na ujenzi wa nyumba.

Jaka Farahani, mkulima wa mwani, alisema changamoto ya masoko inawasumbua sana hasa pale wanunuzi wanaowategemea wasiponunua, hivyo aliiomba wizara kuwasaidia kutatua changamoto hiyo.

Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji (WMUV), Dk. Nazael Madalla, alisema wizara kupitia idara yake inaendelea kuhamasisha kampuni kuendelea kuchukua leseni kwa ajili ya kununua mwani na mpaka sasa zipo kampuni 7. Lengo la kuwa na kampuni nyingi ni kuongeza ushindani hivyo kampuni zinahamasishwa kujisajili ili zitambulike na ziweze kufanya biashara ya mwani.

Scanned with CamScanner

# UFUGAJI BORA WA SAMAKI KATIKA BWAWA

Ufugaji wa samaki: ni shughuli ya kuwaweka na kuwatunza samaki katika bwawa kwa kanuni za ufugaji bora wa samaki ili wapatikane pale watakapohitajika kwa ajili ya chakula au biashara.

**Kanuni za ufugaji bora wa samaki:**
1. kuchagua eneo bora linalofaa kuchimba bwawa la samaki
2. kupima na kuchimba bwawa kwa namna sahihi
3. kujaza maji yasiyo na madhara katika bwawa la kufugia
4. kupandikiza samaki kwenye bwawa na kuwatunza vizuri
5. kutunza bwawa lisiharibike kwa mmomonyoko au magugu
6. kuvua samaki bwawani muda wa kufanya hivyo unapowadia
7. kutayarisha na kuhifadhi samaki kwa namna inayofaa
8. kuuza samaki na kutunza kumbukumbu za shughuli zote

**Athari za kutofuata kanuni za ufugaji bora**

**Kuchagua eneo linalofaa**

Kutofuata kanuni hii, matokeo yake ni kuchimba bwawa mahali ambapo halitadumu, kwa kuingiliwa na mafuriko au kukosa chanzo cha maji ya kujaza bwawa.

**Kupima na kuchimbwa bwawa kwa usahihi**

Matokeo yake ni kuchimba bwawa visivyo na kutofikia kikamilifu kwa lengo la ufugaji samaki

**Kujaza maji yasiyokuwa na madhara**

Kutofuata kanuni hii, matokeo yake ni kupata hasara kwa samaki kudhurika na kushindwa kufikia lengo.

**Kupandikiza samaki na kuwatunza**

Kutofuta kanuni hii, matokeo yake ni samaki kudhurika na kufa kwa kukosa matunzo .

**Kutunza bwawa lisiharibike:**

Kwenda kinyume na kanuni hii, matokeo yake ni bwawa kubomoka na kuchafuka kutokana na magugu na takataka.

**Kuuza samaki na kutunza kumbukumbu:**

Kutofuata kanuni hii, matokeo yake ni kupata hasara ya kukosa mapato na kutojua hasara na faida ya shughuli iliyofanyika.

**Vifaa**

a. Zana za kufyekea na kuchimbia kama panga, jembe, chepe na toroli
b. Zana za kupimia kama kamba, futikamba, mambo na nyundo.
c. Zana za kutengeneza wigo kama nguzo, fito, misumari na waya
d. Chanzo cha maji ya uhakika na yasiyo na madhara kwa samaki
e. Samaki wadogo wa kupandikizwa katika bwawa
f. Vifaa vya kubebea samaki wa kupandikizwa katika bwawa
g. Zana za kufulia samaki kama nyavu, ndoano na mitumbwi

Eneo linalofaa kuchimba bwawa la kufugia samaki
1) Pawe tambarare penye udongo wa mfinyanzi
2) Pasiwe bongeni panapoathiriwa na mafuriko nyakati za mvua
3) Pasiwe na miti mikubwa wala mawe makubwa
4) Pawe karibu na nyumbani kwa urahisi kwa urahisi wa huduma na ulinzi

**Hatua za ufugaji bora wa samaki**

a) Baada ya kupata eneo linalofaa kuchimba bwawa, tuande zana za kufyekea na kuchimbia, chanzo cha maji na mahali pa kupata samaki wa kufuga
b) Tusafishe eneo la kuchimba bwawa kwa kufyeka vichaka vya miti na nyasi ndefu, kung'oa visiki na mizizi yote na kutupa nje ya eneo na kufukia mashimo ya visiki vilivyochimbuliwa
c) Tupime eneo la kuchimba bwawa, kisha tuchime bwawa, kisha tuchimbe bwawa kwa kufuata ushauri na maelekezo ya mtaalamu wa ufugaji wa samaki
d) Tuinue tuta la kingo za bwawa kiasi cha kutosha kisha tupande nyasi katika tuta lote kuzunguka bwawa, ili kuzuia mmomonyoko wa udongo wakati wa mvua na upepo
e) Tuweke chujio mahali mfereji unapoingilia bwawani, ili lichuje na lizuie uchafu usiohitajika kuingia bwawani
f) Weka sehemu ya kutolea maji bwawani ili kupunguza maji bwawa linapojaa na lisifurike wakati wa mvua samaki wakatoka
g) Jaza maji katika bwawa na kuliacha bila kupandikiza samaki kwa muda wa wiki moja

**Jinsi ya kutunza bwawa la kufugia samaki**

A Kagua tuta la bwawa kila mara hasa wakati wa mvua, kama kuna uharibifu wowote katika kuta za tuta ushughulikiwe haraka
B. Ziba sehemu zilizomomonyoka udongo na panda nyasi mahali ambapo nyasi zilizopandwa zimekufa au kuondoka na mmomonyoko.
C. Kagua na ondoa uchafu unaoziba kwenye chekeche za chujio katika sehemu za kuingizia na kutolea maji bwawani.
D. Chunguza na dhibiti wanyama kama vile kenge, nyoka, kobe na vyura na wengineo wanaokula samaki
E. Hakikisha uzio kuzunguka eneo la bwawa ni imara ili kuzuia wanyama na wanadamu kutumia maji ya bwawa kwa kuoga, kunywa na kucheza ndani yake.

**Jinsi ya kuvuna na kuhifadhi samaki**

Baada ya kugundua kwamba samaki ni wakubwa wa kutosha kutumiwa kwa chakula unaweza kuwavua kiasi unachohitaji kwa ndoano, wavu wa mkono au kimia kutegemeana na ukubwa na kina cha bwawa. Kama bwawa ni kubwa na lina kina kilefu zana kama mitumbwi au maboti zinaweza kutumika. Vua samaki wa kutosha mahitaji tu, hifadhi wengine kidogo kwa matumizi ya baadaye kwa kukausha kwa jua, moto, moshi, jokofu au kuwapaka chumvi na kuwaanika.

Ni bora samaki usiowahitaji ukawaacha waendelee kuishi bwawani mpaka muda mwingine, kuliko kuwavua na kuwatoa majin wakafa na kuoza wasikunufaishe kwa kutohifadhiwa vizuri.

**Kumbukumbu za ufugaji wa samaki**

Uwekaji wa kumbukumbu kwa shughuli yoyote inayofanywa ni muhimu ili kuweza kutathimini shughuli hiyo. Hivyo, kwa ufugaji wa samaki ni lazima kumbukumbu za kuanzia matayarisho mpaka mwisho wa ufugaji wa samaki zihifadhiwe ili kubaini mapato na matumizi na gharama nyingine. Pia zitasaidia kujua faida na hasara ya kifedha kama ufugaji unafanywa kwa ajili ya biashara.

Mfano wa Kumbukumbu ya ufugaji wa samaki:

| Tarehe ya kupandikiza | gharama | | Tarehe ya kuvuna | idadi | mauzo | faida |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | ununuzi | vyakula | | | | |
| 20-11-2009 | 20000 | 10000 | 30-11-2011 | 5000 | 58000 | 28000 |

**Uvuvi wa samaki kwa nyavu:**

Namna za kuwategea na kuwanasa samaki zipo nyingi lakin katika somo hili tutajifunza jinsi ya kuvua samaki kwa kutumia nyavu. Uvuvi hufanyika baharini, ziwani, bwawani na hata mitoni.

**Vifaa:**

(a) Vyombo vya kusafiria
(b) Nyavu kamili za matundu yanayokubalika kisheria
(c) Karabai kama uvuvi unafanyika usiku
(d) Visu vya kusafishia samaki
(e) Chambo cha kuvutia samaki
(f) Vyombo vya kuhifadhia samaki

**Jinsi ya kuvua samaki kwa nyavu**

**1. Uvuvi kwa nyavu za kutega**

Nyavu za kutega ni kama vile jarife ambapo nyavu hutengwa zikining'inia majini kusubiri samaki wanase.

**2. Uvuvi wa nyavu za kitanda**

Nyavu za kitanda ni uvuvi ambapo wavuvi hutupa nyavu baharini ili kuwatanda samaki na kuwavua. Nyavu hizi zinakuwa duara ambalo huwazingira samaki wakashindwa kutoroka na kuvuliwa.

**3. Uvuzi wa nyavu wa kuzingira**

Wavuzi hingia katika dau wakiwa na nyavu za kuvulia, chambo, karabai na vyombo vya kuhifidhia samaki na kuelekea sehemu ya uvuvi. Mtumbwi mdogo hufungwa kwa kamba nyuma ya dau lililobeba wavuvi ili ukokotwe. Wakifika eneo la uvuvi taa huwashwa na kuachwa iwake kwa kiasi cha nusu saa hivi. Samaki huvutiwa na mwanga wa taa na hapao huanza kuvua.

**4. Uvuvi kwa nyavu za kukokota**

Nyavu za kukokota huwa zinakokotwa na dau au chombo cha kuvulia kwa masafa fulani katika eneo lenye samaki lililokusudiwa huku chombo kikiwa katika mwendo mdogo na nyavu zikivutwa kidogokidogo kuelekea chomboni.

Kuhifadhi samaki

Baada ya samaki kuvuliwa na kuletwa nchi kavu, watahifadhiwa kwa namna kadhaa ambazo mazingira ya wavuzi hao yataruhusu.

Samaki wanaweza kuhifadhiwa wakakaa muda mrefu bila kuharibika kwa kugandishwa katika majokofu, kupakwa chumvi na kuanikwa juani, kwa kuwabanika kwa moto au kuwakausha kwa moshi.

Ni vyema samaki wanaohifadhiwa kwa chumvi, jua, moto au moshi wakachanwa na kukunjuliwa ili chumvi, joto na moshi viingie ndani ya nyama ya samaki kwa urahisi. Samaki wanaohifadhiwa kwa kupasuliwa kutiwa chumvi na kuanikwa juani hiutwa ng'onda. Baada ya kukauka vizuri, ng'ona wanaweza kukaa bila kuharibika kwa mwaka mzima na wakafaa kwa chakula.

Scanned with CamScanner